TASAFIC

Elimu na Umoja Tuijenge Tanzania

2025

Tanzania Students Associations Federation in China| c/o. Tanzania Embassy in Beijing 8 LiangMa He Nan Lu, Sanlitun, 100600 Beijing, P.R. CHINA| TASAFICtc@gmail.com

Kwa habari zaidi www.TASAFIC.com

# TASAJI Yawaaga Wahitimu kwa Sherehe ya Kipekee Mjini Changchun

Katika majira ya kiangazi mwaka 2025, Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania Jimbo la Jilin (TASAJI) iliandaa hafla ya kuwaaga rasmi wahitimu waliokamilisha masomo yao nchini China. Tukio hilo lililofanyika jijini Changchun, lilikutanisha wanafunzi wote wa Kitanzania kutoka vyuo mbalimbali vya mji huo pamoja na wageni kutoka mataifa tofauti.

Katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa TASAJI, Ndugu Isack Ibrahim Mrisho, alitoa hotuba iliyogusa nyoyo za wengi. Alieleza kuwa TASAJI ni kiungo muhimu cha mshikamano miongoni mwa wanafunzi wa Kitanzania na mataifa mengine wanaoishi Jilin. “TASAJI si chombo cha Watanzania pekee, bali ni daraja linalowaunganisha wanafunzi wote wa Changchun bila kujali asili yao,” alisisitiza.

Kwenye sherehe za mahafali ijayo, Mrisho alipendekeza sherehe ziwe za kimataifa zaidi kwa kushirikisha wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika na mabara mengine, ili kuendeleza misingi ya mshikamano, upendo, na kusaidiana, maadili yanayotambulika na kuheshimiwa ndani na nje ya Tanzania.

Hotuba hiyo ilishangiliwa kwa makofi kutoka kwa hadhira, huku wageni wakisifu moyo wa ushirikiano ulioonyeshwa na TASAJI. Ilikuwa siku ya kumbukumbu, iliyojaa furaha, shukrani na matumaini ya mustakabali mwema wa mshikamano wa wanafunzi wa Afrika na ulimwengu kupitia jumuiya za wanafunzi kama TASAJI.







Wahitimu kutoka vyuo mbalimbali vya Changchun wakikata keki ya Pamoja, ishara ya mshikamano na upendo waliojenga katika safari yao ya kitaaluma nchini China.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania Jimbo la Jilin (TASAJI), Ndg. Isack Ibrahim Mrisho (kulia), alitoa hotuba fupi yenye msukumo wa mshikamano na uongozi bora. Akiwa ameambatana na Makamu Mwenyekiti, Ndg. Glory Azaeli Munisi, aliongoza zoezi la kugawa vyeti kwa wanafunzi walioonyesha ushiriki na mchango wao katika shughuli za kijumuiya na kitaaluma.



Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya TASAJI, Ndg. Glory Azaeli Munisi, akimkabidhi cheti cha pongezi mhitimu Ndg. Daudi Sahani kutoka Chuo Kikuu cha Northeast Normal, Changchun



Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya TASAJI, Ndg. Glory Azaeli Munisi, akimkabidhi cheti cha pongezi kwa mhitimu Mkutoka Chuo cha Changchun Aviation University, kama ishara ya kutambua juhudi na mafanikio yake katika masomo na shughuli za kijumuiya.



Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania Jimbo la Jilin (TASAJI), Ndg. Glory Azaeli Munisi, akikabidhi cheti cha pongezi kwa mhitimu kutoka Tanzania, Ndg. William Chitalika, kwa kutambua mchango wake katika masomo na uongozi wa kijumuiya.




Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania Jimbo la Jilin (TASAJI), Ndg. Glory Azaeli Munisi, akikabidhi cheti cha pongezi kwa mhitimu kutoka Tanzania, Ndg. Abdulkarim Mtoro



Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania Jimbo la Jilin (TASAJI), Ndg. Glory Azaeli Munisi, akikabidhi cheti cha pongezi kwa mhitimu kutoka Tanzania, Ndg. Abel Magembe, ikiwa ni sehemu ya sherehe za kuwapongeza wahitimu kwa mafanikio yao kitaaluma.



Mwanajumuiya wa TASAJI, Ndg. Samwel Muharagi (kulia), mwanafunzi wa shahada ya uzamivu (PhD), akiwa kwenye picha ya pamoja na wanafunzi kutoka Lesotho na Zambia—wakidhihirisha mshikamano wa wanafunzi wa Afrika nchini China



Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania Jimbo la Jilin (TASAJI), Ndg. Glory Azaeli Munisi, akikabidhi cheti cha pongezi kwa mhitimu kutoka Tanzania, Ndg. Emmanuel Lutema, kama sehemu ya kutambua juhudi na mafanikio yake katika masomo na maisha ya kijamii nchini China.



Wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali ikiwemo China, Bangladesh, na Korea wakifurahia sherehe za mahafali iliyoandaliwa na Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania Jimbo la Jilin (TASAJI), tukio lililoakisi mshikamano wa kimataifa na utamaduni wa ujirani mwema



Baadhi ya wanajumuiya wa TASAJI wakiwa pamoja na wanafunzi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), wakionesha mshikamano na urafiki wa kimataifa miongoni mwa wanafunzi wa Afrika walioko Changchun

# Fahari ya Utamaduni wa Tanzania Yang'ara SWUFE – Culture Day Festival

Kilele cha Culture Day Festival 2025 katika Chuo Kikuu cha Southwestern University of Finance and Economics (SWUFE), Chengdu, Sichuan, kiligeuka kuwa jukwaa la kuangaza haiba ya utamaduni wa Kitanzania. Katika hafla hiyo, wanafunzi wa Tanzania walionesha upekee wa urithi wao kupitia mapishi, mila, na mawasiliano ya kijamii, wakichora taswira mpya ya ushirikiano wa kimataifa kupitia utamaduni.

Tukio hilo lilifanyika katika kampasi ya Liullin, na kuwavutia wanafunzi kutoka mataifa mbalimbali walioko nchini China, kila mmoja akiwasilisha sura ya nchi yake. Banda la Tanzania liliwavutia wengi kwa mandhari na ladha halisi ya nyumbani. Harufu ya ndizi nyama, mandazi na pilau iliwanasa wahudhuriaji mbali kabla hata hawajaufikia meza ya chakula, na kuwaalika kwenye safari ya ladha isiyosahaulika ya Kitanzania.

Lakini haikuwa tu kuhusu ladha. Wanafunzi wetu walijitokeza kama mabalozi wa utamaduni, wakifafanua historia na desturi za Kitanzania kwa wageni. Mijadala iliyoibuka iligusa umuhimu wa kuenzi na kushirikisha tamaduni mbalimbali ndani ya jamii ya kimataifa. Picha mbalimbali zilionesha wageni kutoka kila pembe ya dunia wakifurahia chakula chetu, wakitabasamu kwa kuridhishwa na ubunifu wa wapishi wetu.

Licha ya kuwa mbali na nyumbani, ari ya uzalendo na ubunifu wa wanafunzi wa Tanzania haikufifia. Kwa njia ya maelezo ya kina, mapishi ya kipekee, na ukarimu wa asili, waliwakilisha taifa lao kwa fahari na heshima. Hafla hii imethibitisha kuwa popote walipo, Watanzania wanabeba utambulisho wa taifa lao—si kwa maneno tu, bali kwa matendo yenye mvuto na maana.

Utamaduni wetu, fahari yetu hata ughaibuni.




TASAFIC MAGAZINE
JUNE 2025

TASAFIC MAGAZINE
JUNE 2025



Tamasha la Utamaduni SWUFE 2025: Wanawake na wanaume wa Kitanzania wakiupeleka ujumbe wa amani na mshikamano kupitia dansi, mavazi na vicheko katika ardhi ya Sichuan, China.




Aliyevaa vazi la kimasai ni Ndugu James, Mwenyekiti mstaafu wa wanafunzi wa Tanzania Jimbo la Sichuan, akiwa pamoja na Ndugu Hamad Abdalla wakikamilisha maandalizi ya mwisho ya banda la maonesho la Taifa la Tanzania katika Tamasha la Utamaduni la SWUFE 2025.


TASAFIC MAGAZINE
JUNE 2025






TASAFIC MAGAZINE
JUNE 2025

TASAFIC MAGAZINE
JUNE 2025

# Tanzania Yaonyesha Upekee Katika Maadhimisho ya Siku ya Utamaduni

Katika maadhimisho ya *Siku ya Utamaduni* yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Beijing Normal, wanafunzi wa Kitanzania walijitokeza kwa umahiri, wakiiwakilisha nchi yao kwa mvuto wa kipekee kupitia banda lililobeba taswira halisi ya urithi wa nyumbani. Kupitia vipeperushi vya vivutio vya utalii, maelezo ya historia tajiri na vielelezo vya turathi za taifa, walifanikiwa kuwasilisha simulizi ya Tanzania kwa njia iliyojaa haiba.

Maadhimisho hayo yalianza kwa sherehe rasmi ya kupeperusha bendera za mataifa shiriki. Wanafunzi wa Tanzania walijipambanua kwa kuvaa mavazi ya asili kama vitenge, kanga, na mashuka ya Kimasai—mavazi yaliyoibua hisia za heshima na kuvutia hisia za fahari miongoni mwa walimu, wageni waalikwa na familia za wenyeji waliokusanyika kushuhudia tukio hilo.

Katika viwanja vya maonesho, burudani mbalimbali kutoka mataifa tofauti zilinogesha tamasha hilo: ngoma, muziki na sanaa ya asili vikitawala jukwaa. Hata hivyo, banda la Tanzania lilibaki kivutio kikuu, likiwakaribisha wageni kwa vyakula vya asili kama wali wa nazi, sambusa, maandazi na kahawa halisi ya Kitanzania. Ladha hizo ziliwachochea wageni si tu kufurahia, bali pia kujifunza kuhusu maisha, mila na falsafa ya Watanzania.

Mmoja wa wanafunzi waliokuwa mstari wa mbele katika maandalizi alieleza kuwa dhamira yao kuu ilikuwa kuonesha kuwa utamaduni wa Tanzania ni hai, unavutia na unafungamana na watu wa mataifa yote. Kupitia mawasiliano ya moja kwa moja kati ya wanafunzi na wageni, ujumbe huo ulipokewa kwa furaha na mshangao.

Maadhimisho haya yamedhihirisha kuwa, hata wakiwa mbali na ardhi ya nyumbani, wanafunzi wa Kitanzania wana uwezo na moyo wa kuwakilisha taifa lao kwa uzalendo, ubunifu, na mshikamano usiofungwa na mipaka ya bara.




Siku ya Utamaduni ilifunguliwa kwa tukio la kupeperusha bendera za nchi shiriki, ambapo Furaha Myota aliipeperusha bendera ya Tanzania kwa fahari, kama ishara ya ushiriki rasmi wa nchi yetu katika maonyesho ya utamaduni kwa mwaka huu


TASAFIC MAGAZINE
JUNE 2025




Watumishi wa Chuo Kikuu cha Beijing Normal pamoja na wageni waalikwa wakifuatilia kwa makini tukio la kupeperusha bendera za mataifa shiriki, huku jukwaa likiendelea na maonesho ya tamaduni mbalimbali. Ngoma za asili, muziki wa kitamaduni na sanaa za jukwaani zilichukua nafasi ya kipekee kuonesha urithi wa kila taifa.






TASAFIC MAGAZINE
JUNE 2025



Baadhi ya Watanzania katika picha ya pamoja na Profesa Ye wa Chuo Kikuu cha Beijing Normal, mbele ya banda la Tanzania katika maadhimisho ya Siku ya Utamaduni. Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watanzania Beijing, Ndugu Mohamed Chuma (kushoto), aliongoza ujumbe huo huku wakiwa wamevalia mavazi ya asili kama vitenge, kanga na mashuka ya Kimasai.




Ndugu Amadeus Komu na Simon wakiwa katika majukumu ya kuitangaza Tanzania na utamaduni wake. Banda la Tanzania liliendelea kuvutia wageni wengi waliokuja kufurahia vyakula vya asili, huku mabango yakionesha vivutio vya utalii, mavazi ya jadi na historia ya taifa letu.

## Heshima kwa Wahitimu: TA-Nanjing Yatambua Mchango wa Wanajumuiya

Jumuiya ya Wanafunzi wa Tanzania Nanjing iliandaa hafla mahsusi ya kuwatunuku vyeti wahitimu wa mwaka 2025 kama ishara ya kutambua ushiriki na mchango wao katika maisha ya jumuiya kipindi chote cha masomo yao. Tukio hilo lilijaa haiba ya kipekee, likiwa ni kielelezo cha namna jumuiya hiyo inavyothamini uaminifu, uwajibikaji na mshikamano wa wanachama wake. Kupitia makabidhiano hayo, TA-Nanjing iliweka alama ya heshima kwa kila mhitimu aliyeonesha moyo wa kujitolea, ikisisitiza umuhimu wa kujenga urithi wa kijumuiya unaovuka mipaka ya taaluma na muda.




Wahitimu wa mwaka 2025 wakipokea vyeti vyao katika hafla maalum iliyoandaliwa na TA-Nanjing tarehe 14 Juni 2025, kama ishara ya kutambua ushiriki na mchango wao katika jumuiya wakati wa masomo yao mjini Nanjing.



TASAFIC MAGAZINE
JUNE 2025




Viongozi wa TA-Nanjing wakiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wahitimu wa mwaka 2025, kama sehemu ya kumbukumbu ya hafla ya utoaji wa vyeti. Kutoka kushoto: Ndg. Zikomo Gaudence (Mhazini), Ndg. Baraka Bunini (Katibu Mkuu). Kutoka kulia: Ndg. Noel Mlay (Mwenyekiti) na Dkt. Berson Peter Mugaka (Mgeni Rasmi na Mwenyekiti wa zamani wa TA-Nanjing, 2017).




Mgeni rasmi, Dkt. Berson Peter Mugaka, akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa mwaka 2025 kama ishara ya kutambua mchango na ushiriki wake katika Jumuiya ya TA-Nanjing wakati wa masomo yake.




Bi. Asha Khatibu Iddi, Mhazini mstaafu wa TA-Nanjing kwa mwaka 2023/2024, akipokea cheti chake kama kutambua mchango wake kwa jumuiya wakati wa kipindi chake cha uongozi.



TASFIC MAGAZINE
JUNE 2025

## KAMATI ILIOANDAA JARIDA LA TASAFIC JUNE 2025



Heda Augustino Chale, Mwenyekiti

Msimamizi wa makala



Isack Ibrahim Mrisho, M/Mwenyekiti

Mwandishi wa makala



Martin Faustin Itangaja, Katibu

Mhariri wa makala



Zaitun Abubakari, Mjumbe

Mkaguzi wa makala



Delvina Meshili, Mjumbe

Mkaguzi wa makala



Damari Madar Jeremiah, Mjumbe

Mkaguzi wa makala



Neema Oberlin, Mjumbe

Mkaguzi wa makala



Jotham Josephat Kimondo

Mkaguzi wa makala



Gloria Michael Meiseyeki

Mkaguzi wa makala